# JARIDA LA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA

*01 Aprili - Juni 30 2024 | Toleo la 1*













Tovuti yetu: www.mbingadc.go.tz

Fuatilia kurasa zetu mbingadc



Jarida hili la kila robo ya mwaka limedhamiria kusogeza utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kwa wananchi na wadau mbalimbali, Karibu Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwa uwekezaji katika sekta za Kilimo cha mazao ya biashara na chakula kama mahindi na kahawa na Uchimbaji wa madini kama Makaa ya mawe, Dhahabu na vito.

*Mhe. Desderius Haule.*
Mwenyekiti wa Halmashauri,
**Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.**



Jarida hili la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ni chombo cha kuhabarisha umma juu ya utekelezaji wa Mpango mkakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na Selikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikijumuisha tathimini ya miradi na maendeleo ya miradi

*Ndugu. Joseph Kashushura Rwiza.*
Mkurugenzi Mtendaji,
**Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.**

## TIMU YA WAHARIRI

Picha, Habari, Maelezo na Usanifu zimefanywa na :
**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.**

## Yaliyomo:


- Tahariri na yaliyomo …………………………………………………………… ……………………………… i
- Waganga wafawidhi simamieni mapato ………………………………………………… ……………….Uk 1
- Ziara ya Kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango (FUM) …..………………. ……….…………..…..Uk 2
- Mkurugenzi Rwiza na agizo la first aid kit shuleni ……………………………… ………………… Uk3
- Bilioni 1.3 uboreshaji wa miundombinu ya elimu Sekondari … ……………….. ………………. Uk 4
- Tutaendelea kutenga fedha kutekeleza miradi ………………………………………… ………….. .Uk 5
- Watendaji wa kata , vijiji someni taarifa za mapato na matumizi. .. …………………………….Uk 6
- Mkurugenzi Mkuu wa TPHPA atembelea Mbinga ……………………………… ……………….. Uk 7
- Mbinga Dc yapongezwa utekelezaji wa miradi …………………………………… ………..…... Uk 8
- Mkurugenzi Rwiza awapiga msasa wanafunzi……………………………….. ……………… Uk 9
- Uwanja wa Amanimakoro wafaa maonesho ya Nanenane kimkoa 2024 …………………. . Uk 10
- Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura Rwiza ameongoza kikao cha kujengeana uwezo juu ya mchakato wa uundwaji wa sheria ndogo........................ Uk 11
- TAYARI TUMEUPOKEA! Mwenge wa Uhuru 2024 ……………………………………… ……. .Uk 12
- Kifahamu Kikundi Cha Umoja Wa Wanawake Mbalawala …………………………..……… ……Uk 13
- Habari picha ……………………..………………………………………………..………………… …. Uk 14
- Shamba la miti Ndengu ……………………………………………………………………………..…… Uk 15
- Mkurugenzi Kashushura ataka kituo cha afya kukamilika kwa wakati ………………… .......... Uk 16
- Mkurugenzi Kashushura akagua miradi ya TASAF ……………………………… ..............…. Uk 17
- Mbinga Dc yapokea Bil. 1.2 ujenzi wa miundombinu ya elimu…………………….. …………. Uk 18
- Hospitali Ya Halmashauri Ya Wilaya Ya Mbinga ……………… ………………………………… Uk 19
- Kituo Cha Afya Matiri ………………………………………………………………………………...……Uk 21
- Shule mpya ya Sekondari Kitumbalomo …………………………………………………... ……… Uk 22
- Nyumba ya Walimu (two in one) Shule ya Sekondari Mndeme ……………..……… ..........… Uk 23
- Ujenzi wa Bweni la wanafunzi Shule ya Sekondari Hagati. ………………………… ………..... Uk 24



# WAGANGA WAFAWIDHI SIMAMIENI MAPATO



**Na Silvia Ernest.**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Rwiza ametembelea na kukagua ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya unaotekelezwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. mnamo tarehe18 Aprili 2024

Baadhi ya majengo aliyotembelea katika hospitali hiyo ni pamoja na jengo la utawala, maabara, jengo la kufulia pamoja na jengo la mama na mtoto.

Aidha Mkurugenzi Rwiza ametembelea na kukagua ujenzi wa jengo la makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambao upo katika hatua za ukamilishaji.

Lengo la ziara hiyo ni kuimarisha usimamizi katika utekelezaji huo ambao utakwenda kuleta tija kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kama ilivyo azma ya Serikali.



Kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango (FUM) imefaanya ziara ya kumetembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga tarehe 06 Mei 2024

**Na Silvia Ernest.**

Katika ziara hiyo kamati imetembelea ujenzi wa nyumba 3 za Wakuu wa idara ambazo zinagharimu Tshs. 360,274,650, ambapo kiasi cha Tshs. 240,000,000 fedha kutoka Serikali Kuu na Tshs. 120,274,650 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri.

Vilevile kamati imekagua ujenzi wa wodi 3 za kulaza wagonjwa ( wanawake, watoto na wanaume) zinazojengwa katika hospitali ya Halmashauri ambapo ujenzi huo utagharimu kiasi cha Tshs.500,000,000.

Aidha kamati imetembelea ujenzi wa bweni shule ya Sekondari Hagati ambao utagharimu kiasi cha Tsh. 128,000,000 pamoja na ujenzi wa bweni la wasichana Shule ya Msingi Maguu ya wanafunzi wenye mahitaji maalam 128.





# MKURUGENZI RWIZA NA AGIZO LA FIRST AID KIT SHULENI

**Na Silvia Ernest.**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Rwiza amewataka Walimu Wakuu wa shule za Msingi na Wakuu wa shule za Sekondari zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kuhakikisha wanaweka kisanduku cha huduma ya kwanza( First Aid Kit) shuleni ili kuwezesha utoaji wa huduma ya kwanza kwa wanafunzi.

Agizo hilo limetolewa tarehe 19 Aprili 2024 katika kikao kazi cha Mkurugenzi Mtendaji na walimu Wakuu na Wakuu wa Shule, Maafisa Elimu Kata, Maafisa Tarafa pamoja na Watendaji wa Kata.

" Uwepo wa first aid kit katika shule zetu ni muhimu sana katika kutoa huduma ya kwanza kwa wanafunzi wetu pindi dharula inapotokea ,kwahiyo kila Mkuu wa shule ahakikishe anatekeleza hili" Amebainisha Mkurugenzi Rwiza.

Ili kuhakikisha wanafunzi wanaongeza maarifa na ustadi amewataka walimu hao kuanzisha na kuendeleza klabu mbalimbali katika shule zao akisisitiza kuwa ni mfumo mzuri wa kuwajengea uwezo pamoja na kuwaongezea maarifa wanafunzi.

" Kuna Klabu kama za mazingira, Rushwa na nyingine nyingi anzisheni hizi Klabu na kama zipo basi ziendelezeni zina faida kubwa kwa wanafunzi"Amesisitiza.

Aidha katika kuhakikisha miradi ya maendeleo inakamilika kwa wakati na katika ubora tarajiwa amewataka washiriki wa kikao hiko kushirikiana kwa pamoja katika utekelezaji wa miradi pamoja na kuhakikisha kila mmoja anatimiza majukumu yake ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi.

Kwa upande wa Maafisa Elimu Kata, Mkurugenzi Rwiza amewataka maafisa hao kutimiza wajibu wao wa kusimamia na kufuatilia masuala ya taaluma katika maeneo yao lengo likiwa ni kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

# BILIONI 1.3 UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU SEKONDARI

**Na Silvia Ernest.**

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu katika shule za Sekondari zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Taarifa hiyo imetolewa na Kaimu Afisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Rashid Bundala katika Kikao kazi cha Walimu Wakuu,Wakuu wa Shule, Maafisa Elimu Kata, Watendaji wa Kata pamoja na Maafisa Tarafa kilichofanyika 19 Aprili 2024.

Amebainisha kuwa kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri Shilingi Milioni 184 zinatekeleza ujenzi wa matundu 8 ya vyoo katika shule ya sekondari Namswea, ujenzi wa matundu ya vyoo 12 katika shule ya Sekondari Mkumbi pamoja na ujenzi wa matundu 6 ya vyoo katika shule ya Sekondari Luhagara.

"Ukamilishaji wa Chumba cha Tehama na vyumba vya maabara Shule ya Sekondari Mndeme, ukamilishaji wa bweni shule ya Sekondari ya wavulana Mbinga, ukamilishaji wa nyumba ya walimu shule ya Sekondari Benaya ,ujenzi wa matundu ya vyoo 8 katika Shule ya Sekondari Nyoni pamoja na ujenzi wa matundu 6 ya vyoo Sekondari ya Kipololo " Amebainisha Bundala.



Bundala ameeleza kuwa Serikali kupitia mradi wa Secondary Education Quality Improvement Programme (SEQIP) imetoa shilingi bilioni 1.1 kutekeleza ujenzi wa shule mpya ya sekondari Kitumbalomo, ujenzi wa bweni shule ya sekondari Hagati,ukamilishaji wa vyumba 3 vya madarasa shule ya sekondari Hilela, ukamilishaji wa vyumba 2 ya madarasa katika shule ya sekondari Kipapa pamoja na ujenzi wa nyumba ya walimu shule ya sekondari Mndeme.

Aidha amebainisha kuwa Serikali kupitia mradi wa Education perfomance for results ( EP4R) imetoa kiasi cha shilingi milioni 176 kutekeleza ujenzi wa bweni 1 na utengenezaji wa vitanda 40( double decker) katika shule ya Sekondari Ruanda pamoja na ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule ya Sekondari Ruanda.



Picha ya kwanza na ya pili zikionyesha Maafisa Elimu Kata, Wakuu wa Shule na wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Katika Ukumbi wa Shule ya Sekondari Kigonsera.
**19 Aprili 2024**




# TUTAENDELEA KUTENGA FEDHA KUTEKELEZA MIRADI" HAULE

**Na Silvia Ernest.**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Mhe.Desderius Haule amebainisha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga itaendelea kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji na utekelezaji wa miradi mipya itayokwenda kuleta tija kwa wananchi.

Haule amebainisha hayo tarehe 13 Mei 2024 akijibu swali la Diwani wa Viti maalum Kata ya Kihangimahuka Mhe. Leonora Mwinuka katika mkutano wa baraza la madiwani kujadili taarifa za robo ya tatu kuanzia mwezi Januari hadi Machi 2024 lililouliza Je Halmashauri ina mkakati gani wa kukamilisha miradi viporo.

Haule ameeleza kuwa pamoja na shughuli nyingine utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni kipaumbele cha Halmashauri katika kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande wake Katibu wa Baraza hilo Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Rwiza ametoa rai kwa madiwani kushirikiana na wataalam wa Halmashauri katika kukusanya mapato ili fedha hizo zitumike katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Aidha amebainisha kuwa pamoja na vyanzo vya mapato vilivyopo,Halmashauri inaendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza mapato pamoja na kuondokana na utegemezi wa fedha



Akitoa salamu za Serikali, Mkuu wa Wilaya ya Mbinga Mhe. Kisare Makori amempongeza Mkurugenzi Mtendaji kwa kusimamia ukusanyaji wa mapato na kuvuka lengo la makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Akichangia mada katika Mkutano huo Diwani wa Kata ya Matiri Mhe. William Mbwambo ametoa rai kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kuona namna bora ya kuwafikia wanawake wengi zaidi wakati wa zoezi la uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi.



# WATENDAJI WA KATA , VIJIJI SOMENI TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI.

**Na Silvia Ernest.**

Watendaji wa Kata na Vijiji wametakiwa kuhakikisha taarifa za mapato na matumizi zinatolewa kwa wananchi kupitia vikao vya kisheria ili kuleta uwazi na uelewa wa pamoja wa matumizi ya fedha katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Agizo hilo limetolewa tarehe 14 Mei 2024 na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Rwiza alipozungumza na wananchi wa Kijiji cha Luhagara Kata ya Litumbandyosi. " Kila mtendaji katika halmshauri hii anatakiwa kusoma taarifa ya mapato na matumizi, wananchi wana haki ya kujua namna fedha zinavyotumika katika maeneo yao" Amebainisha.

Pia ametumia nafasi hiyo kuwataka Wakuu wa shule na Walimu wakuu kufuatilia mahudhurio ya wanafunzi na kuhakikisha idadi ya wanafunzi wanaoanza elimu ya msingi au sekondari inalingana na idadi ya wanafunzi watakaohitimu.






**Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mbinga Joseph Rwiza amekutana na kuzungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viatilifu Tanzania (TPHPA)**



**Na Silvia Ernest.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mbinga Joseph Rwiza amekutana na kuzungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viatilifu Tanzania (TPHPA) Prof. Joseph Ndunguru.
Lengo la mazungumzo hayo ambayo yamefanyika katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga tarehe 29 Mei 2024 ni kuona namna bora ya kuboresha sekta ya kilimo na kupanga mipango ambayo itasaidia kuleta maendeleo endelevu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.



# MBINGA DC YAPONGEZWA UTEKELEZAJI WA MIRADI

**Na Silvia Ernest.**

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas amempongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Rwiza kwa kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Halmashauri pamoja na ujenzi wa wodi tatu katika hospitali ya Halmashauri ya Wilaya.

Pongezi hizo zimetolewa tarehe 29 Mei 2024 katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga

"Utekelezaji wa miradi unaridhisha nikupongeze Mkurugenzi maboresho madogo madogo ni kama kupanda miti ya matunda miti ya kivuli ili eneo hili livutie" Amesema

Sambamba na pongezi hizo ametoa wito kwa Halmashauri kuhakikisha miundombinu hiyo inatunzwa vizuri na kusisitiza kuwa Serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Kwa kipekee Kanali Abbas amempongeza Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu na Maendeleo ya Vijiji na Miji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Bi. Neema Mbilinyi kwa kusimamia utekelezaji miradi, amemtaka kuendeleza ari hiyo ya kutekeleza miradi katika viwango bora.

**" Mimi binafsi nina farijika sana nikikuta Mhandisi anaesimamia ujenzi ni mwanamke, umefanya kazi nzuri inaonekana endeleza hiyo ari ya uwajibikaji na uzalendo"** Amesisitiza

Ujenzi wa jengo la makao Makuu ya Halmashauri umegharimu shilingi Bil 3.3 hadi kukamilika na ujenzi wa wodi tatu utagharimu shilingi 500,000,000 hadi kukamilika.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga inaendelea kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji huo ambao unakwenda kuleta tija kwa wananchi.



# MKURUGENZI RWIZA AWAPIGA MSASA WANAFUNZI.

**Na Silvia Ernest.**

Mkurugenzi mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Rwiza amewataka wanafunzi wote kuzingatia masomo na kutambua jitihada zinazofanywa na wazazi wao za kuhakikisha wanapata elimu bora.

Aidha amewataka kutambua azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kuimarisha na kuboresha sekta ya elimu nchini.

Rwiza ametoa wito huo tarehe 14 Mei 2024 alipozungumza na wanafunzi wa shule za Sekondari Ruanda na Litumbandyosi katika ziara yake ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo.


" Nafasi hii mlioipata itumieni vizuri wazazi wanataka mpate elimu bora lakini pia Rais wetu amewekeza fedha nyingi ili tujifunze katika mazingira rafiki" Amebainisha Rwiza

Sambamba na hilo Mkurugenzi Rwiza ametoa wito kwa watoa huduma za afya kulinda na kutunza miundombinu ya kutolea huduma za afya akisisitiza kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi katika miundombinu hiyo.

" Hivi vifaa tulivyoletewa tuvitunze ili vitumike kwa muda mrefu lakini tuhakikishe mazingira yanayotuzunguka yanakuwa safi na yanapendeza" Amesisitiza Rwiza

Katika ziara hiyo Mkurugenzi Rwiza ametembelea kituo cha afya Litumbandyosi, shule za sekondari Ruanda na Litumbandyosi pamoja

# UWANJA WA AMANI MAKORO WAFAA MAONESHO YA NANENANE KIMKOA 2024



**Na Silvia Ernest.**

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas amethibitisha kuwa uwanja wa maonesho ya Nane Nane Amani Makoro uliopo Kata ya Amani Makoro Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga unafaa kwa ajili ya maadhimisho ya sherehe za nane nane Mkoa wa Ruvuma kwa mwaka 2024.

Ameahidi kwenda kulifanyia kazi ombi la Mkuu wa Wilaya ya Mbinga Mhe. Kisare Makori la kuomba maadhimisho hayo Kimkoa yafanyike katika uwanja huo.

Hayo yamebainishwa tarehe 30 Mei 2024 katika ziara ya Mkuu wa Mkoa kutembelea na kukagua miundombinu ya uwanja huo.

Aidha ameagiza miundombinu ya viwanja hivyo iendelee kuboreshwa ili kama itaamriwa maadhimisho hayo yafanyike katika viwanja hivyo, tayari mazingira yawe rafiki.

"Viwanja hivi vinafaa nimengalia mazingira yapo rafiki na nimesikia ombi la Mkuu wa Wilaya la kuomba mwaka huu Kimkoa maadhimisho yafanyike katika eneo hili sasa nipeni muda nikafanye maamuzi kati ya hapa na viwanja vya Sinai" Amesisitiza

Akisoma taarifa Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mhandisi Evance Haule amesema Uwanja huo ambao upo Kilomita 8 kutoka barabara kuu ya Mbinga- Songea una ukubwa wa ekari 18.8 ulitolewa na wananchi wa Kijiji cha Amani Makoro kupitia Serikali ya Kijiji kwa ajili ya maonesho hayo.

Haule ameeleza kuwa mpangilio wa matumizi ya viwanja katika eneo hilo unahusisha viwanja vya mabanda ya maonesho ya kilimo na mifugo, Wajasiriamali, Huduma za kijamii,Taasisi za Serikali na binafsi, Bustani, Maegesho ya magari, Uwanja wa mikutano, Eneo la burudani pamoja na matumizi mengineyo.




**Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura Rwiza ameongoza kikao cha kujengeana uwezo juu ya mchakato wa uundwaji wa sheria ndogo.**

Na Silvia Ernest.

Kikao hicho ambacho kilifanyika tarehe 1 Juni 2024 kimelenga kuleta uelewa wa pamoja juu ya umuhimu wa sheria ndogo na mchakato wa uundwaji au utengenezaji wa sheria ndogo ambazo zitatekelezwa katika Halmashauri.



# TAYARI TUMEUPOKEA!







**Na Silvia Ernest.**

Mkoa wa Ruvuma unatarajia kukimbiza Mwenge wa Uhuru umbali wa Kilomita 1,289.50.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas tarehe 8 Juni 2024 katika mapokezi ya mwenge wa Uhuru yaliyofanyika katika Kijiji cha Sauti Moja Wilaya ya Tunduru.

" Katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Mwenge wa Uhuru utakimbizwa KM 284, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo KM 170, Halmashauri ya Wilaya ya Songea KM 134.8, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga KM 110.30, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa KM 186.6, Halmashauri ya Mji Mbinga KM 140.5, Halmashauri ya Manispaa ya Songea KM 98.20 na Halmashauri ya Wilaya ya Madaba KM 165.10" Amebainisha Kanali Abbas

Kanali Abbas ameongeza kuwa jumla ya miradi 72 yenye thamani ya shilingi 46,101,114,953.76 iliyopo ndani ya Mkoa wa Ruvuma itafikiwa na Mwenge wa Uhuru.

" Miradi 17 itafunguliwa yenye thamani ya 5,714,686,491.95, miradi 13 itawekwa jiwe la Msingi yenye thamani ya 10,604,369,677.69 na miradi 42 itatembelewa yenye thamani ya shilingi 29,782,085,784.12" Amebainisha



# KIFAHAMU KIKUNDI CHA UMOJA WA WANAWAKE MBALAWALA

**Na Silvia Ernest.**

Kikundi cha Umoja wa wanawake Mbalawala kinachojishughulisha na uzalishaji na uuzaji wa Nishati ya makaa yame kwa ajili ya kupikia ni miongoni mwa mafanikio ya mkopo wa 10% unaotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwa wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu.2020

Kikundi kilianza kutekeleza mradi wake kwa gharama ya Tshs. 130,000,000 kati ya hizo kiasi cha Tshs 30,000,000 ni mkopo 10% kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mwaka 2020 na kiasi cha shilingi 100,000,000 ni nguvu za wanachama wa kikundi na msaada kutoka kwa mdau TANCOAL ENERGY.

Kikundi hiki kina uwezo wa kuzalishatani 4 za nishati ya makaa ya mawe kwa siku na nishati hiyo ikiuzwa kwa bei ya Tshs. 400 kwa kilo moja,imebanishwa kuwa mauzo ya nishati hiyo kwa siku ni Tsh 1,600,000 na kufanya jumla ya Tshs. 153,000,000 kwa mwaka.

Kupitia makusanyo hayo kikundi kimeweza kurejesha mkopo wa 10% pamoja na kuzalisha ajira kwa vijana 10 ambao kati yao wenye sifa ya shahada ni 7 ambao wanajishughulisha na kazi za Maabara, uzalishaji na masoko.



# HABARI PICHA



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mbinga Joseph Rwiza akikagua utekelezaji wa miundombinu katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Tarehe 18 Aprili.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mbinga Joseph Rwiza akikagua shamba la miti la Ndg. Festo Mhagama lilipo katika Kijiji cha Mabuni Kata ya Litumbandyosi tarehe 14 Mei 2024.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mbinga Joseph Rwiza ujenzi wa madarasa mawili Shule ya Sekondari Ruanda tarehe 14 Mei 2024.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Juhudi iliyopo katika Kata ya Kigonsera wakifanya usafi ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili 2024.




Mkurugenzi Mtendaji Joseph Rwiza akizungumza na wananchi kupitia Radio Hekima juu ya ujio wa Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga tarehe 11 Juni 2024.



# SHAMBA LA MITI NDENGU

Shamba la Miti la Ndengu lenye ukubwa wa Ekari 240 Linamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga likiwa na miti aina ya Mipaina na Milingoti.Lilianza kupandwa mwaka kwa awamu tokea mwaka 1963 na kuanza kuvunwa mwaka 2010 mpaka 2013,
Baada ya hapo miti ilirejeshwa kwa kupandwa kwa awamu tokea mwaka 2010 mpaka 2018.

Shamba hili ni muhimu kwa mifumo kiikolojia kama utunzaji wa vyanzo vya maji vya miti ya Bonde la Ziwa Nyasa na Mto Ruvuma, kuzuia mmomonyoko wa udongo na sehemu ya uwekezaji wa kibaiolojia kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

***"Tunza mazingira yakutunze, Ilinde misitu dhidi ya moto"***





# MKURUGENZI KASHUSHURA ATAKA KITUO CHA AFYA KUKAMILIKA KWA WAKATI

**Na Silvia Ernest.**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura amemtaka Mkurugenzi wa Kampuni ya ujenzi SAM Contrators Ndg. Muhidin Milanzi kuhakikisha anakamilisha ujenzi wa Kituo cha afya Nyoni kwa wakati na katika ubora.

Mkurugenzi Kashushura ametoa agizo hilo katika ziara yake ya kukagua utekelezaji huo tarehe 19 Juni 2024.

" Ujenzi huu hakikisha unakamilika kwa wakati ili Kituo kianze kutoa huduma kwa wananchi, lakini tekeleza katika ubora ili hata zikitokea fursa nyingine ni rahisi kupata kutokana na uaminifu wako"

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kampuni ya SAM Contractors Ndg. Muhidin Milanzi ameahidi kuwa ifikapo tarehe 20 Julai 2024 ujenzi utakuwa umekamilika.

" Naelewa azma ya Serikali kuwa wananchi wapate huduma bora za afya katika maeneo yao na sio kwenda mbali Nikuhaidi Mkurugenzi Kituo hiki kitakamilika kwa wakati na kwa ubora zaidi"

Aidha amemshukuru Mkurugenzi Kashushura kwa kutumia muda wake kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi hatua ambayo inapelekea kurahisisha utekelezaji.

Kituo cha Afya Nyoni kinajengwa kupitia mapato ya ndani na hadi kukamilika ujenzi huo utagharimu shilingi Mil.500





# MKURUGENZI KASHUSHURA AKAGUA MIRADI YA TASAF

**Na Silvia Ernest.**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura amefanya ziara ya kutembelea na kukagua miradi inayotekelezwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii / TASAF.

Lengo la ziara hiyo ni kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa katika ubora kama ilivyo azma ya Serikali.


Katika ziara yake ametembelea mradi wa barabara wenye kivuko unaotekelezwa katika Kijiji cha Likwela Kata ya Nyoni barabara inayoanzia Tundu A kwenda Tundu B.

Aidha ametembelea maradi wa ukarabati wa barabara wenye mita 900 ambao unatekelezwa katika Kijiji cha Kihulila Kata ya Nyoni barabara inayoanzia Kihulila rami kwenda shule ya Msingi Ndesa.

Pia ametembelea mradi wa miti 5000 unaotekelezwa katika Kijiji cha Mitawa kata ya Mpapa.



# MBINGA DC YAPOKEA BIL. 1.2 UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU MKURUGENZI KASHUSHURA ATOA RAI KWA WATAALAMU.



**Na Silvia Ernest**

Kufuatia mapokezi ya fedha shilingi 1, 268, 752,825 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Elimu Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Mkurugenzi Joseph Kashushura amewataka wataalamu wanaosimamia utekelezaji huo kuimarisha usimamizi wakati wote wa utekelezaji.

Mkurugenzi Kashushura ametoa rai hiyo katika kikao cha kupokea taarifa ya mapokezi ya fedha kilichofanyika tarehe 28 Juni 2024 katika ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

"Tufanye kazi tupate matokeo yanayoridhisha tumepokea fedha lakini ni wajibu wa kila mmoja katika nafasi yake kutimiza wajibu ili miradi ikamilike kwa wakati na thamani ya fedha ionekane" Amebainisha

Akitoa taarifa ya mapokezi hayo Kaimu Afisa Elimu Sekondari Rashid Bundalah amebainisha kuwa kiasi cha Tshs. 655,552,827 kimepokelewa kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa SEQUIP.

" Shilingi 560,552,827 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Kata ya Muungano na Shilingi 95,000,000 kwa ajili ya nyumba ya walimu (two in one) shule ya Sekondari Kitumbalomo" Amebainisha Bundalah

Kwa upande wa Elimu Msingi Kaimu Afisa Elimu Yunus Salum amesema Shilingi 613,200,000 zimepokelewa kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa BOOST kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, matundu ya vyoo pamoja na ukarabati wa shule za msingi Mhongozi, Lotoho, Ukata, Limboni pamoja na Lunoro na fedha hizo tayari zimeingizwa katika akaunti za benki za shule husika.






# HOSPITALI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA

**Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga**
**Gharama:** shilingi Bilioni 2.550 fedha kutoka Serikali Kuu
**Majengo:** Jengo la wagonjwa wanje (OPD), Maabara, jengo la Wazazi, Kichomea taka, Jengo la kufulia, jengo la mionzi pamoja na wodi tatu( wanawake, wanaume,watoto) pamoja na Bohari ya Dawa .





# KITUO CHA AFYA MATIRI



**Ujenzi wa Kituo cha Afya Matiri**
**Gharama:** Milioni 563 fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri
**Majengo:** Jengo la wagonjwa wan je (OPD), Maabara, jengo la Wazazi pamoja na Kichomea taka.







# KITUO CHA AFYA MKUMBI

**Ujenzi wa Kituo cha afya Mkumbi**
**Gharama:** Milioni 500 fedha kutoka Serikali Kuu
**Majengo:** Jengo la wagonjwa wanje (OPD), Maabara, jengo la Wazazi pamoja na Kichomea taka.







## Shule mpya  ya Sekondari
# Kitumbalomo

**Gharama:** Milioni 742,509,996.8( mapato ya ndani  181,957,169.8, mradi wa SEQIP 560,552,827)
**Mwaka:** 2022/2023







## Nyumba ya Walimu (two in one) Shule ya Sekondari Mndeme

**Ujenzi wa nyumba ya Walimu (two in one) Shule ya Sekondari Mndeme**
Gharama: **M**ilioni 95 fedha kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa SEQUIP
Mwaka: 2022/2023





**Jarida hili limetolewa na Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini**
**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashuri ya Wilaya ya Mbinga**
239 Barabara ya Mbambabay, S. L. P 194, 57483 kigonsera – Ruvuma.
Simu +255 (025) 2640005, Nukushi +255 (025) 264004
Barua pepe: ded@mbingadc.go.tz, Tovuti: www.mbingadc.go.tz